# HOTUBA YA WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI MHESHIMIWA DAVID MATHAYO DAVID (MB), KWENYE UFUNGUZI WA MKUTANO WA KWANZA WA BARAZA LA NNE LA MWAKA LA WADAU WA TASNIA YA NYAMA TANZANIA, TAREHE 29 FEBRUARI 2012 GLONENCY 88 HOTEL, MOROGORO

Mhe. Joel N. Bendera, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro
Dkt. Charles Nyamrunda, Katibu Mkuu, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi,
Dkt. Ben Moshi, Mwenyekiti wa Baraza la Mwaka la Wadau wa Tasnia ya Nyama,
Prof. Faustin Lekule, Mwenyekiti wa Bodi ya Nyama Tanzania,
Ndugu Wawakilishi wa Wizara na Taasisi za Serikali,
Ndugu Wawakilishi wa Taasisi zisizo za Kiserikali (NGO),
Ndugu Wajumbe wa Baraza la Mwaka la Wadau wa Tasnia ya Nyama,
Ndugu Wajumbe wa Bodi ya Nyama Tanzania,
Wageni Waalikwa,
Mabibi na Mabwana.

**Ndugu Mwenyekiti**,
Awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kukutana hapa siku ya leo tukiwa na afya njema. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kushukuru uongozi wa Mkoa wa Morogoro kwa mapokezi mazuri waliyotupatia. Pia kuwapongeza na kuwashukuru waandaaji wa mkutano huu kwa kunialika kuja kufungua mkutano huu muhimu, wa Baraza la Mwaka la Wadau wa Tasnia ya Nyama linalosimamia maendeleo ya tasnia ya nyama nchini.

Vile vile, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwenu wote kwa kuitikia mwaliko wa kushiriki katika mkutano huu licha ya majukumu makubwa mliyonayo. Hii inadhihirisha ni kwa kiwango gani Wadau wa tasnia ya Nyama nchini mmedhamiria kuleta mapinduzi ya kweli katika maendeleo ya Tasnia. Vile vile, natoa pongezi kwa Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kupendekeza na kuwawezesha wajumbe walioteuliwa kushiriki katika mkutano huu muhimu. Napenda kuchukua nafasi hii kuziagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa nyingine ambazo hazijawakilishwa kuiga mfano huu na kuwezesha wadau wake kuwakilishwa katika mkutano huu muhimu kwa maendeleo ya tasnia ya nyama.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Nimeambiwa kwamba Baraza hili ni la Pili kuteuliwa tangu kuzinduliwa kwa Baraza la Mwaka la Wadau wa Tasnia ya Nyama Nchini. Hivyo, napenda kukupongeza kwa dhati Mwenyekiti

kwa kuteuliwa kwako kuliongoza Baraza hili. Hii inatokana na mchango wako mkubwa ulioonyesha katika kuendeleza tasnia ya nyama na kwamba Taifa lina imani kuwa kwa kushirikiana na wajumbe wa Baraza mtaleta mabadiliko makubwa katika tasnia hii. Aidha, napenda kuwapongeza wajumbe wa Baraza jipya kwa kuteuliwa kwenu kuwa wawakilishi wa wadau wa maeneo mnayotoka katika baraza hili. Ni matumaini yangu kuwa mtashiriki vema katika kutekeleza majukumu yenu na kufanikisha malengo ya Baraza. Nina imani kuwa mtaweza kutoa mrejesho kwa wadau waliowatuma kuhusu maazimio ya mkutano na kuhamasisha utekelezaji wake. Hivyo, nawatakia nyote kwa ujumla kazi njema.

**Ndugu Mwenyekiti,** ili kuleta mapinduzi katika maendeleo ya sekta ya mifugo, utekelezaji wa shughuli mbalimbali umeendelea kufanyika kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025; Malengo ya Kimataifa ya Millenia (MDGs) na Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA). Katika kutekeleza malengo ya Millenia (MDGs), sekta ya mifugo inatakiwa kuchangia katika kupunguza umaskini takribani kwa asilimia 50 ya wananchi wasiokuwa na chakula cha kutosha na wenye kipato cha chini ya dola moja kwa siku ifikapo 2015.

Kwa upande wa MKUKUTA, sekta ya mifugo inatarajiwa kukua kutoka asilimia 2.3 mwaka 2009 hadi asilimia 4.5 mwaka 2015 ili kuchangia kikamilifu kwenye Pato la Taifa. Wizara imeendelea kuhakikisha malengo niliyoyataja yanafikiwa kwa kuendelea kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP), Azma ya Kilimo Kwanza, Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006, na kuandaa Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo ya mwaka 2010 na Programu ya Kuendeleza Sekta ya Mifugo ya mwaka 2011. Programu hii itakayotekelezwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo tayari imeainishwa katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 -2015/16).

Aidha, Mipango ya kuchochea uwekezaji katika sekta ya kilimo ili kufuta umaskini ijulikanayo kama Mpango wa Uwekezaji katika Kilimo na Uhakika wa Chakula (*Tanzania Agriculture and Food Security Investment Plan* - TAFSIP} na *Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania* (SAGCOT) imezinduliwa. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine imeandaa Mpango wa Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Zao la Nyama Nyekundu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa za Morogoro, Iringa Manispaa, Jiji la Mbeya na Halmashauri za Iringa na Mbeya. Juhudi hizi zitahusisha kujengea uwezo wa kitaalam na kibiashara kwa wanenepeshaji, wafanyabiashara ya mifugo, nyama na mazao yake. Pia, mpango huu utasaidia Mamlaka husika kuweka vifaa vya kuchinja na kupooza nyama katika machinjio. Hivyo, natoa wito kwa wajumbe wa Baraza hili kuhakikisha kuwa mikakati na programu mbalimbali za kitaifa zilizopo zinazolenga kuleta mapinduzi ya kijani katika sekta ya mifugo mnazielewa kikamilifu na kuainisha maeneo ya utekelezaji.

**Ndugu Mwenyekiti,** zipo sheria mbalimbali zinazoongoza tasnia ya nyama ili iweze kuwa na tija. Kuwepo kwa sheria hizi kunachochea kuweka mazingira mazuri kibiashara na kuchochea uwekezaji nchini. Baadhi ya sheria hizo mbali na Sheria ya Nyama Na. 10 ya Mwaka 2006 ni pamoja na Sheria ya Magonjwa ya Mifugo Na. 17 ya Mwaka 2003, Sheria ya Biashara Ngozi Na 18 ya Mwaka 2008, Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya Mwaka 2008, Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo na Mazao yake Na.12 ya Mwaka 2010, Sheria ya Maeneo ya Malisho na Vyakula vya Mifugo Na. 13 ya Mwaka 2010. Pamoja na kuwepo kwa sheria hizi, bado kuna changamoto katika usimamizi na utekelezaji wake na hivyo kuathiri maendeleo ya sekta.

**Ndugu Mwenyekiti,**
Ninaamini kwamba wote tunatambua umuhimu wa Baraza la Mwaka la Wadau wa Tasnia ya Nyama. Baraza hili ni chombo kilichoanzishwa kisheria na kina jukumu la kuhamasisha na kusimamia maendeleo ya tasnia ya nyama na kuhakikisha **Sheria ya Nyama Na. 10 ya Mwaka 2006** pamoja na sheria nyingine zinazoongoza tasnia ya nyama zinatekelezwa. Hili ni jukumu kubwa, ambalo likitekelezwa vema litaleta mabadiliko makubwa katika ufanisi wa tasnia. Hivyo, ni vyema kila Mjumbe wa Baraza hili akafahamu kwa kina majukumu na wajibu wake na kujituma kuyatekeleza. Nimeambiwa kwamba kutakuwepo na warsha itakayotangulia na mada mbali mbali zitawasilishwa, ikiwemo mada ya Sheria ya Nyama Na. 10 ya Mwaka 2006 itakayoeleza majukumu ya Baraza, hivyo sina sababu ya kuyataja tena majukumu hayo hapa ila ninaomba kila mjumbe ajitahidi kuyaelewa majukumu ya Baraza na kuyazingatia. Pamoja na sheria hizo, **Baraza pia linapaswa kufanya kazi kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006, Mkakati pamoja na Programu ya kutekeleza sera hiyo**.

**Ndugu Mwenyekiti,** pamoja na kuwa wajumbe wa Baraza lako wanawakilisha wadau wote wa tasnia ya nyama, ni dhahiri kwamba sehemu kubwa ya wanaowakilishwa ni wafugaji wa asili ambao ni takribani kaya milioni 1.8 wanamiliki rasilimali kubwa ya mifugo zaidi ya asilimia 90. Mifugo hiyo ni pamoja na ng'ombe milioni **21.3,** mbuzi milioni **15.2,** Kondoo milioni **6.4,** nguruwe milioni **1.9** na kuku milioni **58** ambayo mchango wake katika pato la Taifa ni asilimia 4 kwa mwaka. Aidha, kwa takwimu tulizonazo uvunaji wa mifugo mashambani ni kati ya asilimia 4 na 5 kwa mwaka, badala ya kiwango kinachotakiwa cha asilimia 15 – 30 kwa mwaka. Hii inasababishwa na kutovuna mifugo kwa wakati na kutozingatia ubora wa mifugo inayohitajika katika soko. Hatuna budi kuelimishana na kutambua umuhimu wa kuvuna mifugo, hali ambayo itatusaidia kuuza mifugo mingi yenye ubora na bei nzuri kwa mwaka.

**Ndugu Mwenyekiti,** pamoja na utajiri mkubwa wa raslimali ya mifugo iliyopo, bado sekta ya mifugo inakabiliwa na changamoto za uzalishaji, uvunaji na mauzo ya mazao ya mifugo hususan maziwa, ngozi na nyama zinazosababishwa na kosaafu za mifugo ya asili; ukosefu wa ardhi na malisho ya kutosha; ukame wa mara kwa mara; uhaba wa miundombinu ya masoko; uhaba wa huduma za tiba na udhibiti wa magonjwa; pamoja na wadau kutokuwa na habari za kutosha kuhusu mahitaji ya soko la nyama. Aidha, utumiaji wa chini wa uwezo wa machinjio za kisasa na viwanda vya kusindika nyama zimechangia katika kudumaa kwa ufanisi wa tasnia ya nyama nchini.

Pamoja na changamoto hizi, tasnia ya nyama imeendelea kuchangia katika upatikanaji wa chakula, pato la taifa, fedha za kigeni na kuiwezesha nchi yetu kutotumia akiba ya fedha zake za kigeni kuagiza nyama kutoka nje ya nchi. Michango hii inatokana na juhudi za wafugaji wote hususan wafugaji wa asili, wadau wengine na Serikali katika kuendeleza tasnia ya nyama. Napenda kutoa wito kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa hususan zile zilizoko katika kanda zenye mifugo mingi, pamoja na kuendelea kutatua changamoto nyingine, ziangalie kwa jicho la pekee utengaji, upimaji na umilikishaji wa maeneo ya malisho kwa mifugo na kuhakikisha yanatumika vema ili kupunguza migogoro ya ardhi na watumiaji wengine. Halmashauri ziendelee kutoa kipaumbele kwa shughuli za ufugaji na ziweke taratibu nzuri za kuwahamasisha wafugaji kufuga kibiashara na kuvuna mifugo yao kwa wakati.

**Ndugu Mwenyekiti,** takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa nchi yetu imekuwa ikikumbwa na hali ya ukame karibu kila baada ya miaka kumi hivi. Kutokana na mabadiliko ya tabianchi, kwa sasa nchi yetu inakumbwa na ukame baada ya kipindi kifupi. Mathalani, katika kipindi cha miaka minne kati ya mwaka 2006 - 2009, nchi yetu ilikumbwa na ukame mwaka 2006 na mwaka 2009. Mabadiliko ya tabianchi siyo tu yameathiri mifumo ya wafugaji wa asili bali yamesababisha pia kupoteza mifugo mingi na kwa ujumla kuathiri maendeleo ya tasnia ya nyama nchini. Ili kupunguza madhara ya mabadiliko haya, Baraza halina budi kushirikiana na asasi za kijamii kuandaa mikakati itakayowasaidia wafugaji kukabiliana na changamoto hii.

**Ndugu Mwenyekiti,** tutakubaliana kwamba bado kuna fursa kubwa ya kuongeza uzalishaji endapo mbinu za kuendeleza malisho, kufuga mifugo bora zaidi, kudhibiti magonjwa pamoja na kulenga uzalishaji unaozingatia mahitaji ya soko zitazingatiwa. Serikali itaendelea kuhamasisha wadau kuwekeza katika ufugaji wenye tija na wa kibiashara ili kuinua kipato cha wafugaji, hivyo kuchangia katika Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA).

**Ndugu Mwenyekiti,** kwa sasa, soko la nyama la ndani na nje ya nchi limendelea kukua. Soko la Nchi za Falme za Kiarabu ambapo tumekuwa tukipeleka wastani wa tani 34.1 kwa

wiki ya nyama ya mbuzi (tani 27.6), ng'ombe (4.3) na kondoo (2.2). Hivyo, kwa mwaka, tulitakiwa kuuza tani 832 lakini katika mwaka 2010/2011 tumeweza kuuza tani 403.3 za nyama tu (sawa na asilimia 48 ya mahitaji) kwenda nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Kuwait, Oman na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC). Hii ni changamoto nyingine tunayohitaji kuiangalia kwa karibu. Ili kuweza kufikia mahitaji ya masoko hayo hatuna budi kuwa na umoja/ushirika wa masoko ya mifugo kwani soko linahitaji kuhakikishiwa upatikanaji wa nyama yenye ubora sawa kwa kipindi chote cha mwaka jambo ambalo ni vigumu kutekelezwa na mfugaji/mfanyabiashara mmoja mmoja. Ninaamini kuwa wote tunaelewa kuwa nchi yetu imeridhia Itifaki ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki inayolenga kurahisisha uhusiano katika Jumuiya ikiwa ni pamoja na biashara. Ni wajibu wa Baraza hili kuhakikisha tunazalisha mifugo bora itakayowezesha kuzalisha nyama bora inayokidhi viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa na kuingia soko la ushindani la Jumuiya hii.

Serikali kwa upande wake imeendelea kuboresha miundombinu ikiwa ni pamoja na minada ya mifugo ya ndani na mipakani. Hata hivyo, pamoja na kuwepo kwa minada hiyo ya mipakani, wafugaji/wafanyabiashara wamekuwa wakitorosha mifugo kwenda nchi jirani bila kupitia minada iliyopo, jambo linaloisababishia nchi kukosa mapato. Hata hivyo, minada yote inakabiliwa na changamoto ya kuwa na mizani ili kutoa bei zinazowiana na ubora wa mifugo. Ninatoa wito kwa Halmashauri zote nchini kuhakikisha kuwa minada ya mifugo inawekewa mizani na mifugo inauzwa kwa kuzingatia uzito. Ni jukumu la Baraza hili kuhakikisha linahamasisha wafugaji juu ya umuhimu wa kuuza mifugo yao kwa kutumia mizani.

**Ndugu Mwenyekiti,** usindikaji wa nyama na mazao yake hapa nchini umeendelea kuwa wa chini, licha ya Serikali kuendelea kuhamasisha wadau wa sekta kuwekeza katika kujenga machinjio/viwanda vya kusindika nyama na mazao yake. Kwa sasa, hapa nchini, zipo machinjio za kisasa takribani sita katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Morogoro, Pwani na Manyara. Machinjio hizi zina uwezo wa kuchinja ng'ombe kati ya 40 na 200 kwa siku. Kama mtakumbuka wakati wa kufungua Baraza la Mwaka la Wadau wa Tasnia ya Nyama lililomaliza muda, Baraza lilipewa changamoto ya kuona jinsi ya kusaidia viwanda vilivyopo kutumia uwezo wake. Changamoto hii bado inaendelea mpaka sasa ambapo wastani wa usindikaji bado uko chini ya asilimia 50 ya uwezo uliopo. Aidha, machinjio nyingi zilizoko chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeshindwa kuboresha machinjio zake na kuendelea na uchinjaji katika hali isiyoridhisha kiusafi na usalama wa nyama. Nafahamu kwamba Baraza lililopita lilikuwa katika hali ya kujipanga katika kujenga mifumo ya kisera, kisheria na kiutawala. Ni matumaini yangu kuwa Baraza hili kwa kutumia misingi iliyowekwa na Baraza lililopita, litabuni mikakati mipya itakayowezesha kuongeza ufugaji wa kibiashara na kuingia mikataba na wenye viwanda ili kuhakikisha upatikanaji wa mifugo bora ya kuchinja unakuwa endelevu. Aidha, natoa wito kwa wataalam wa mifugo nchini kutumia

ujuzi wao na kuwekeza katika ufugaji wa kibiashara ili kutumia fursa ya kuwepo soko la mifugo na kukuza taaluma kupitia ranchi zao.

**Ndugu Mwenyekiti,** eneo jingine la kuleta mapinduzi ya kijani katika ufugaji wetu ni kubadilisha au kuboresha aina ya mifugo tuliyonayo. Ng'ombe wengi tulionao ni wa asili ambao tija na kiwango cha uzalishaji ni kidogo. Serikali inaendelea kuhamasisha ufugaji wa kisasa katika ranchi, kunenepesha mifugo, kufuata kanuni bora za ufugaji na matumizi ya mbegu za kisasa za mifugo ya nyama. Katika kufanikisha hili, Wizara imeanzisha vituo vipya vya uzalishaji na utunzaji wa hewa baridi ya naitrojeni na mbegu za mifugo wa nyama katika kanda ya Mashariki (Kibaha), Kusini (Lindi), Kati (Dodoma), Ziwa (Mwanza) na Nyanda za Juu Kusini (Mbeya) vitakavyosaidiana na kituo cha Taifa cha Uhimilishaji kilichoko NAIC Arusha katika kusogeza huduma hii ya uhimilishaji kwa wafugaji. Natoa changamoto kwa Baraza hili kuhakikisha wafugaji wanahamasishwa na kubuni mikakati itakayowezesha teknolojia hii inawafikia wafugaji wengi zaidi ili waweze kuzalisha na kuuza mifugo yenye tija na inayokidhi mahitaji na viwango vya soko.

**Ndugu Mwenyekiti**,
Nimepata taarifa za kuanza kwa juhudi za kuunda na kuimarisha ushirika wa kitaifa wa wafugaji, wafanyabiashara na wasindikaji. Huu ni mwelekeo mzuri ambao Baraza lako pamoja na Bodi mnatakiwa kuwa karibu ili kuhakikisha ushirika huu unaanzishwa haraka. Kuanzishwa kwa Ushirika huu kutawaunganisha pamoja wadau wa tasnia ya nyama na kuwawezesha kutetea maslahi yao. Tatizo lililojionyesha katika Baraza lililopita, wajumbe wengi wa Baraza hilo walikuwa wanajiwakilisha wenyewe au vyama ambavyo sio hai hali ambayo isipoangaliwa vizuri inaweza kuendelea hata kwenye Baraza hili. Napenda niliagize Baraza lako kuhakikisha kwamba wajumbe wa Baraza hili wawe wanawakilisha vyama vya wadau wa nyama vilivyo hai na kuhakikisha taarifa za kazi zinazofanywa na vyama hivyo za kuwaletea wanachama maendeleo katika tasnia ya nyama ziwe zinawasilishwa kwenye Bodi ya Nyama.

**Ndugu Mwenyekiti,** Serikali inaendelea na mchakato wa kuanzisha Benki ya Kilimo nchini ambapo kwa sasa, imetoa mtaji katika Benki ya Rasilimali (TIB), kwa ajili ya kutoa mikopo nafuu ya muda mrefu kwa wadau wa sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Wote tunatambua kuwa upatikanaji wa mikopo kwa shughuli za ufugaji kutoka kwenye mabenki ya kibiashara ni moja ya vikwazo vikuu katika kuendeleza sekta ya mifugo nchini. Inakadiriwa kuwa ni asilimia 8 tu ya wadau wanaojishughulisha na kilimo na ufugaji ndiyo wanaopata mikopo ambayo mara nyingi ni ya muda mfupi, riba kubwa na masharti magumu ambayo huwashinda wengi. Natoa wito kwa wataalam na wafugaji kutumia fursa hii kupata mikopo itakayowawezesha kuwekeza katika tasnia ya nyama. Aidha, natoa wito kwa wadau wa

tasnia ya nyama kuanzisha Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOs) ili kuwawezesha wadau kupata mitaji ya kuendeleza tasnia ya nyama na kuongeza mapato ya Taifa kwa ujumla.

**Ndugu Mwenyekiti**, Ninafahamu kwamba Baraza hili litapendekeza majina ya wajumbe wa Bodi kwa mujibu wa Sheria ya Nyama Na. 10 ya Mwaka 2006 watakaowakilisha wadau katika Bodi itakayoteuliwa hivi karibuni kwa kuwa Bodi iliyopo imemaliza muda wake. Naagiza kuwa muwe makini katika kupendekeza wajumbe wa Bodi, wawe ni wale wenye mtazamo na ari ya kuendeleza tasnia kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo. Bodi hii mpya itaundwa katika kipindi chenye changamoto kubwa za kuendeleza tasnia ya nyama, ambazo ni pamoja na kujenga uwezo wa wadau wa kiushindani na kuwezesha biashara halali ya mifugo na nyama katika soko la Afrika Mashariki na Kati pamoja na nchi za Mashariki ya Kati.

**Ndugu Mwenyekiti**, mwisho, napenda kuyawekea mkazo mambo matano yafuatayo:

1. Uzalishaji na uongezaji thamani wa zao la nyama uzingatie viwango vya ubora kwa mujibu wa sheria na kanuni zake. Wadau wazingatie taratibu katika uzalishaji;
2. Vyama vya wadau viundwe, vifufuliwe na kuimarishwa kwa kujengewa uwezo;
3. Kuhamasisha uundaji wa SACCOs ili kutoa fursa ya kupata mitaji;
4. Kuhamasisha wadau kuingia ubia na wawekezaji wengine; na
5. Kuboresha mifugo kwa kutumia uhimilishaji ili kupata mifugo bora.

**Ndugu Mwenyekiti**, natumaini kuwa katika mkutano huu mtakuwa huru na wazi zaidi katika kujadili na kutoa maoni ya namna ya kuboresha na kuleta mapinduzi katika sekta ya mifugo hususan tasnia ya nyama ili sekta hii iweze kuboresha maisha ya wafugaji. Ni matarajio yangu kwamba Baraza hili litatathmini utekelezaji wa yale yaliyoelekezwa katika Mkutano wa Baraza lililopita na kuweka malengo mapya ya Baraza lenu. Vile vile, Baraza hili litatoa maazimio yatakayowezesha kupunguza au kuondoa kabisa vikwazo katika kuendeleza tasnia ya nyama na hivyo kuongeza mchango wake katika pato la Taifa.

Baada ya kusema hayo, napenda sasa kutamka kuwa mkutano wa nne wa Baraza la Mwaka la Wadau wa Tasnia ya Nyama **umefunguliwa rasmi**.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**